Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani:

Majukumu na haki zako

SWAHILI

Novemba 2018

Australian Government
Department of Education and Training

NSW FAMILY DAY CARE ASSOCIATION INC.

MKUSANYIKO WA TAARIFA ZA MWALIMU WA FAMILY DAY CARE:

Majukumu na haki zako

Serikali ya Australia inaidhinisha watoaji wa huduma za utunzaji wa watoto chini ya Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani. Mtoaji huduma aliyeidhinishwa ana kibali cha kuendesha kituo kimoja au zaidi cha huduma.

Kama mwalimu, umeajiriwa na huduma ya Family Day Care - utunzaji unaotoa ni kwa niaba ya kituo hicho cha huduma. Serikali ya Australia inaidhinisha watoaji wa huduma za utunzaji watoto na huduma wanazoendesha chini ya Sheria ya Huduma za Elimu na Utunzaji na Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani.

Ni muhimu ufahamu kwamba Sheria ya Kitaifa na Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani zinadhibiti Family Day Care na ruzuku ambazo familia ambazo zinastahiki zinaweza kupokea kutoka kwa Serikali ya Australia.

Kuna mahitaji kadhaa muhimu ambayo ni lazima uyatimize ili kuhakikisha kuwa wewe na huduma yako ya Family Day Care hamvunji Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani au Sheria na Kanuni za Huduma za Elimu na Utunzaji. Kituo chako cha huduma kinapaswa kukusaidia kuelewa sheria hizi.

Ni lazima uwe na bima

Ni lazima uwe na bima ya dhima ya umma ya angalau milioni $10 ya makazi yako ya Family Day Care na uhakikishe bima yako imesasishwa.

Ni lazima uwe mtu anayefaa kutoa huduma hiyo

Kama mwalimu, ni lazima uwe mtu anayefaa kutoa huduma ya utunzaji wa watoto. Unapaswa kuwa na kibali cha polisi na Kibali cha Kufanya Kazi na Watoto au umetimiza hitaji sawia na hilo. Kituo chako cha huduma ni lazima kiwe kinaweza kutoa rekodi iliyoandikwa ya vibali hivyo, wakati wowote kikiombwa na Idara ya Elimu na Mafunzo.

Mambo yanayohusisha ulaghai, udanganyifu au upuuzaji yanaweza kuathiri iwapo wewe ni mtu anayefaa au asiyefaa. Kanuni za Kitaifa pia zinatumika kwa watu wengine wazima ambao wanaishi na wewe kwa mfano unapaswa kumwarifu mtoaji wako wa huduma ikiwa mtu mzima mgeni anaanza kuishi na wewe. Mtoa Huduma Aliyeidhinishwa ni lazima ahakikishe watu wote wazima katika nyumba yako watu wanaofaa na kustahili kuishi na watoto. Hupaswi kamwe kumuacha mtoto au watoto wakiwa peke yao na wageni.

Unapaswa kuwa na sifa stahiki

Unapaswa kuwa na au unaendelea kupokea sifa stahiki - Cheti cha III katika Huduma za Elimu na Utunzaji. Sifa stahiki hii itakusaidia kuboresha stadi zako za kutoa huduma ya utunzaji na elimu kwa watoto wadogo. Unaweza kusomea Cheti hiki cha III kupitia chuo cha TAFE au katika shirika la mafunzo lililosajiliwa. Unahitaji pia sifa stahiki za huduma ya kwanza ikiwa na pamoja na cheti cha Huduma ya Kurejesha Pumzi Kwa Kubana Kifua na Kupitisha Hewa kwa Pua (CPR) na mafunzo ya udhibiti wa pumu na mzio wakati wa dharura.

Ni lazima uwe umesajiliwa na PRODA

Ni lazima pia uwe umesajiliwa kwa akaunti ya Ufikiaji wa Kidijitali wa Mtoa Huduma (PRODA), na umeunganishwa na mtoa huduma ili Ruzuku ya Utunzaji wa Mtoto ilipwe kwa utunzaji unaotoa kwa familia zako.

Baada ya kujisajili na PRODA na kuthibitisha utambulisho wako, utapokea nambari ya Mamlaka ya Usajili (RA). Unapaswa kupeana nambari hii kwa mtoa huduma wako wa Family Day Care kwa sababu wataihitaji ili kukuunganisha na huduma yao ya Family Day Care kwenye Mfumo wa Ruzuku ya Utunzaji wa Watoto. Unapaswa kufahamu kuwa malipo ya Ruzuku ya Utunzaji wa Watoto hayawezi kutolewa kwa ajili ya utunzaji uliotolewa iwapo mwalimu hajathibitisha utambulisho wake na PRODA na kupeana nambari yake ya RA kwa mtoa huduma wa Family Day Care.

Maelezo ya jinsi ya kukamilisha usajili yapatikana katika **www.education.gov.au/becoming-child-care-subsidy-approved-child-care-service**.

Ni lazima utoe huduma bora

Kama mwalimu, ni lazima utimize Kiwango cha Kitaifa cha Ubora wa Huduma za Elimu na Utunzaji na utumie Mfumo wa Mafunzo ya Miaka ya Awali na Mfumo wa Utunzaji wa Watoto Waliofikisha Umri wa Kwenda Shule ili kuunga mkono utoaji wa utunzaji bora na mafunzo katika mazingira salama.

Umeruhusiwa kutunza idadi fulani tu ya watoto

Unaweza kutunza hadi watoto saba tu wakiwemo jamaa, kwa wakati mmoja (wakiwemo watoto walio na umri wa miaka 13 au chini na wasiohudhuria shule ya upili), na watoto wasiozidi wanne wasiwe wamefikisha umri wa shule ya chekechea au chini yake.

Ni lazima uhakikishe kuwa chini ya 50% ya watoto unaowatunza kwa kila wiki mbili wana uhusiano na wewe.

Huduma inapaswa kuweka kiwango cha ada

Kituo chako cha huduma ya utunzaji kina wajibu wa kuweka kiasi cha ada na kuunda sera za utozaji ada.

Unalipwa na kituo cha huduma, na familia hulipa kituo cha huduma kwa utunzaji wa watoto wao. Malipo yako yanapaswa kunakiliwa katika makubaliano yaliyoandikwa kati yako na kituo chako cha huduma.

Ni muhimu kufahamu kuwa familia hulipa kituo cha huduma na wala hazikulipi moja kwa moja. Walimu wengi hukusanya pesa kutoka kwa familia, hata hivyo, wanapofanya hivyo huwa

wanakusanya kwa niaba ya kituo cha huduma.

Ingawa kituo cha kutoa huduma kinaweza kukuruhusu uweke pesa hizi kama sehemu ya malipo yako kutoka kwa kituo hicho.

Kituo chako cha huduma kinahitajika kutoa hati za kuthibitisha malipo na risiti.

Kituo chako cha huduma kinahitajika kutoa kwa familia hati moja ya kuonyesha malipo na huduma zilizotolewa mara moja kila baada ya wiki mbili. Hati hii ya kuonyesha malipo inawaarifu huduma ambayo imetolewa, ada ambazo zimetozwa na Ruzuku ya Utunzaji wa Watoto au Ruzuku ya Ziada ya Utunzaji wa Watoto ambayo imelipwa.

Kama mwalimu, ni jambo nzuri kutoa risiti wakati unapopokea malipo kutoka kwa familia. Utahitajika kutoa rekodi ya risiti kwa kituo chako cha huduma. Ni lazima risiti zionyeshe kwa uwazi kwamba ada zinalipwa kituo chako cha huduma.

Familia hutoa mchango wa kuongezea kwa ada za utunzaji wa watoto wao kwa kulipa mtoa huduma kiasi cha fedha ambacho ni tofauti kati ya ada inayotozwa na kiasi cha Ruzuku ya Utunzaji wa Watoto. Ili kustahiki kupokea Ruzuku ya Utunzaji wa Watoto, ni lazima familia ziwajibikie malipo ya ada za utunzaji wa mtoto chini ya Makubaliano ya Uzingatiaji Yaliyoandikwa na mtoa huduma ya utunzaji wa watoto.

Unapaswa kulinda rekodi za familia

Taarifa zote kuhusu familia hazipaswi kutolewa kwa watu wengine ila pale ambapo inahitajika chini ya Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani. Adhabu zinatumika kwa matumizi au ufichuaji wa taarifa usio na idhini.

Ni lazima utoe ripoti na rekodi sahihi za mahudhurio kwa kituo chako cha huduma

Kama mwalimu, ni lazima utoe ripoti sahihi za mahudhurio kwa kituo chako cha huduma kuhusu utunzaji unaotoa kila wiki. Hii inamaanisha unapaswa kuripoti mahudhurio ya vipindi ambavyo kwa kweli mtoto alihudhuria. Unaweza kuripoti kesi za kukosa kuhudhuria, lakini iwapo tu mtoto alipaswa kuwa anatunzwa na iwapo tu familia ilitozwa ada ya utunzaji huo.

Ukiwasilisha ripoti za mahudhurio zisizo sahihi kwa kituo chako cha kutoa huduma hii inaweza kusababisha kituo chako au familia kuwa na deni ambayo inahitaji kulipwa siku za usoni.

Je, ni zipi haki zangu kama mwalimu?

Huduma yako ya Family Day Care inapaswa kuweka desturi fanisi na zenye maadili mema ili kukusaidia kama mwalimu.

Desturi fanisi na zenye maadili mema ni pamoja na kutoa taarifa kwa walimu kwa wakati unaofaa na mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma, kuhimiza umoja na ushirikiano, na kuendeleza na kufuata viwango vya kitaaluma na kanuni za maadili.

Mambo Muhimu

- Serikali inatoa Ruzuku ya Utunzaji wa Watoto na Ruzuku ya Ziada ya Utunzaji wa Watoto kwa familia zinazostahiki zinazotumia huduma za Family Day Care chini ya Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani.
- Kituo chako cha huduma kina majukumu ya kisheria chini ya Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani na Sheria ya Kitaifa.
- Unahitaji sifa stahiki rasmi ili uwe mwalimu na unafaa kutoa utunzaji bora na mafunzo katika mazingira salama ukitumia Mifumo ya Mafunzo inayokubalika.
- Ni lazima uwe umesajiliwa kwa akaunti ya Ufikiaji wa Kidijitali wa Mtoa Huduma (PRODA), na umeunganishwa na mtoa huduma ili Ruzuku ya Utunzaji wa Watoto ilipwe kwa utunzaji unaotoa kwa familia zako.
- Unaweza kutunza hadi watoto saba tu kwa wakati mmoja (walio na umri wa miaka 13 au chini na wasiohudhuria shule ya upili), na watoto wasiozidi wanne wasiwe wamefikisha umri wa shule ya chekechea au chini yake, na chini ya 50% ya watoto wenye uhusiano na wewe.
- Huduma yako ya Family Day Care ndiyo inayoweka kiwango cha ada. Unaweza kukusanya pesa kutoka kwa familia lakini haya ni malipo ya kituo cha huduma – ingawa kituo cha huduma ya utunzaji kinaweza kukuacha uweke pesa unazokusanya kama sehemu ya malipo yako kutoka kwa kituo cha huduma.
- Ni jambo nzuri kutoa kwa familia risiti sahihi ambazo ni lazima zionyeshe wazi kuwa ada zinalipwa kwa kituo chako cha huduma ya utunzaji.
- Mipangilio ya malipo yako inapaswa kunakiliwa katika makubaliano yaliyoandikwa kati yako na kituo chako cha huduma.
- Ni lazima kituo chako cha huduma ya utunzaji kitoe hati za kuonyesha malipo na huduma zilizotolewa na risiti kwa familia mara moja kila baada ya wiki mbili.
- Ni lazima utoe ripoti sahihi za mahudhurio ya watoto kwa kituo chako cha huduma ya utunzaji. Ni lazima utoe rekodi za mahudhurio zilizotiwa sahihi za kila mtoto anayehudhuria kipindi cha utunzaji, zikiwemo rekodi za kipindi chochote ambacho mtoto hakuhudhuria.
- Iwapo unatoa rekodi za mahudhurio zisizo sahihi kwa kituo chako cha huduma ya utunzaji, unavunja sheria.



This brochure has been produced in 11 languages: Amharic, Arabic, Assyrian, Dari, Dinka, French, Hazaragi, Nuer, Somali, Sudanese, and Swahili. To find the brochure in your language please go to **www.fdcsupport.org.au**

Haki ya kufahamishwa

Kama mwalimu, unapaswa kupokea taarifa sahihi na zilizosasishwa, hasa kuhusu masuala yanayoathiri mazingira yako ya kazi. Kituo chako cha huduma ya utunzaji kinapaswa kuwa na sera na taratibu zilizo wazi ili kuhakikisha kuna matarajio sawia kuhusu jinsi mambo yanavyofanywa katika kituo cha huduma na kuendeleza desturi yenye upatanifu.

Haki ya Mafunzo ya Kujiendeleza Kitaaluma

Kusasisha na kudumisha ujuzi wa walimu ni jukumu la pamoja la walimu, waratibu, na kituo cha huduma ya utunzaji wa watoto. Unapaswa kupewa fursa za mara kwa mara ili kuhudhuria mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma ili kukusaidia kuwa mwalimu bora na kuhakikisha unaelewa sheria na kanuni ambazo ni lazima kuzifuata.

Viwango vya kitaaluma na kanuni za maadili

Kituo chako cha huduma ya utunzaji, walimu na wahudumu wanapaswa kutumia desturi zenye maadili mema na viwango vya kitaaluma katika kufanyia maamuzi na kuongoza mienendo katika huduma yao. Kanuni ya maadili ni sheria ya desturi ambayo inaainisha maadili ya huduma yako ya Family Day Care na kutoa matarajio wazi ya majukumu yako katika mahusiano yenu na ya familia na watoto wanaotumia huduma hiyo.

Huduma yako ya Family Day Care inapaswa kuwa na Kanuni ya Maadili ya Usalama wa Mtoto ili kuondoa wasiwasi kuhusiana na tabia gani inayofaa au isiyofaa kwa watoto wa kituo chako huduma ya utunzaji.

Ikiwa kama mwalimu wa Family Day Care una matatizo na viwango vya kitaaluma au unaamini kuwa umelipwa kiasi kisicho sahihi na kituo chako cha huduma ya Family Day Care, unapaswa kujadili hili na kituo chako.

Amharic በራስዎ ቋንቋ በራሪ ወረቀት ለማግኘት **www.fdcsupport.org.au**. ድረ ገጽን ይመልከቱ

Arabic لإيجاد الكتيب بلغتك، يُرجى تصفح موقع الويب **www.fdcsupport.org.au**.

Assyrian ܠܡܫܟܚܘܬܐ ܕܗܢܐ ܟܬܒܘܢܐ ܒܠܫܢܘܟ݂ܘܢ، ܒܥܝ ܡܢܘܟ݂ܘܢ ܚܙܘ݂ ܕܣܚܪܘ ܠܣܐܝܬ **www.fdcsupport.org.au**.

Dari برای دریافت جزوه به زبان خودتان، لطفاً به ویبسایت **www.fdcsupport.org.au** مراجعه کنید.

Dinka Të kɔɔr yin kitap në thoŋdu kitam tɔ̈ wëlthin ke yin lɔ në **www.fdcsupport.org.au**.

French Pour trouver la brochure dans votre langue, veuillez visiter le site **www.fdcsupport.org.au**.

Nuer Kɛ ɣöö bi ŋäc jiek rɛy warɛgakä/ kiɛ majalɛ kɛ thuok du, göa ɛ ɛn ɣöö bi wä kä **www.fdcsupport.org.au**.

Hazaragi برای دریافت این بروشور به زبان خود تان، لطفاً به ویب سایت **www.fdcsupport.org.au** مراجعه کنید.

Somali Si aad ugu heshid buugyaraha luuqadaada fadlan booqo **www.fdcsupport.org.au**.

Sudanese لإيجاد الكتيب بلغتك، الرجاء تصفح موقع **www.fdcsupport.org.au**.

Swahili Ili kupata brosha hiyo kwa lugha yako tafadhali tembelea tovuti **www.fdcsupport.org.au**.

FAHAMU MENGI ZAIDI

Mwongozo wa Mtoa Huduma ya Utunzaji wa Watoto ni rasilimali muhimu kwa watoa huduma wa mafunzo ya watoto wachanga na utunzaji wa watoto na inaweza kupatikana katika:

www.education.gov.au/child-care-provider-handbook-0

Fahamu mengi kwa kutembelea tovuti zifuatazo:

- **www.education.gov.au/compliance**
- **www.education.gov.au/child-care-providers**
- **www.fdcsupport.org.au**
- **www.fdca.com.au**
- **www.acecqa.gov.au**

Au kwa kutembelea tovuti ya huduma yako ya Family Day Care au kwa taarifa nyingine yoyote ambayo wametoa kama vile vijitabu vya maelekezo au miongozo ya jinsi ya kuanza.

Novemba 2018

Australian Government
Department of Education and Training

NSW FAMILY DAY CARE ASSOCIATION INC.
since 1976